

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE
IDARA YA ELIMU MSINGI
TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA IDARA KWA KIPINDI CHA
MWEZI JANUARI-MACHI 2021.**

1.0: UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya mlele ina tarafa moja yenye jumla ya kata sita za kielimu, vijiji kumi na nane (**18**) na shule kumi na tisa (**19**). Halmashauri ya wilaya ya mlele ina jumla ya wanafunzi **17676**, wakiwemo wavulana **9037** na wasichana **8639**. Ina idadi ya walimu **183**, wanaume **146**, na wanawake 37.

2.0 IDADI YA WANAFUNZI NA WALIMU HADI MACHI 31 2020

NA	HALMASHAURI	JINA LA SHULE	IDADI YA WANAFUNZI (awali-vii)			WALIMU					
			WAV	WAS	JML	MAHITAJI	WALIOPO			UPUNGU FU	PTR
							ME	K E	JM		
1	MLELE	INYONGA	995	1014	2009	41	11	13	24	17	1:77
2	MLELE	KALOVYA	532	544	1076	21	9	3	12	9	1:80
3	MLELE	KAMALAMPAKA	666	683	1349	26	8	0	8	18	1:143
4	MLELE	NSENKWA	587	586	1173	22	12	2	14	8	1:72
5	MLELE	MTAKUJA	410	373	783	15	10	1	11	4	1:60
6	MLELE	MGOMBE	1468	1360	2828	57	15	4	19	38	1:134
7	MLELE	WACHAWASEME	247	216	463	9	6	2	8	1	1:53
8	MLELE	KUSA	320	354	674	14	8	1	9	5	1:72
9	MLELE	ILELA	374	350	724	14	10	1	11	3	1:56
10	MLELE	MAPILI	738	714	1452	28	9	5	14	14	1:91
11	MLELE	MASIGO	216	218	434	8	8	1	9	0	1:41
12	MLELE	KAMSISI	1334	1252	2586	52	23	1	24	28	1:98
13	MLELE	ILUNDE	1150	975	2125	43	17	3	20	23	1:97
	JUMLA		9037	8639	17676	351	146	37	183	168	

2.0: SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA IDARA MWEZI JANUARI-MACHI, 2021.

1. Kuratibu na kusimamia masuala ya taaluma katika shule za Msingi.
2. Kusimamia ujenzi wa miundombinu katika shule za Msingi.
3. Kushughulikia urekebishaji wa takwimu za wanafunzi katika mfumo wa PREMS
4. Kusimamia na kuratibu usajili wa shule sita (06) za Msingi
5. Kusimamia na kuratibu utengenezaji wa madawati ya wanafunzi wa shule za Msingi.
6. Kuratibu na Kusimamia zoezi la kuendelea kuchukua tahadhali ya magonjwa ya mlipuko hasa ugonjwa wa Covid 19.
7. Kuratibu ufanyikaji wa mtihani wa majaribio ngazi ya Kata kwa madarasa ya mitihani (darasa la saba) pamoja na ufanyikaji wa mitihani kabla ya likizo fupi ya pasaka 2021.
8. Kusimamia uandikishaji wa darasa la awali, la kwanza na MEMKWA.
9. Kusimamia na kushiriki katika zoezi la kufanya tathimini ya matokeo ya darasa la saba ya mwaka 2020 Mkoani.
10. Kufuatilia zoezi la ufunguaji shule za Msingi kwa muhula wa kwanza 2021.
11. Usajili wa watahiniwa watakaofanya mtihani wa kumaliza elimu ya Msingi 2021 na watakao fanya upimaji wa kitaifa darasa la nne.
12. Kuratibu na kusimamia masuala ya taaluma katika shule za Msingi.
13. Kusambaza fomu za ufundishaji shuleni kupitia kwa waratibu wa elimu kata
14. Shule zote kumi na tisa zimejaza fomu za ufundishaji kupitia kwa Waratibu Elimu Kata(MEK) na kuwasilisha ngazi ya Halmashauri kwa ufuatiliaji zaidi.
15. Kuanza ukataji wa Magogo kwa ajili ya utengenezaji wa Madawati ya shule za Msingi
16. Kuratibu na kusimamia maandalizi ya UMITASHUMTA

4.0 CHANGAMOTO

- Upungufu wa Walimu, walimu wanaohitajika 351, waliopo 183 pungufu 168.
- Upungufu wa vyumba vya madarasa, yanayohitajika ni madarasa 351, yaliyopo 140, pungufu 211.
- Upungufu wa nyumba za walimu, yanayohitajika ni nyumba 183, zilizopo 58, Pungufu 125.
- Uhaba wa vifaa vya kufundishia wanafunzi wenye mahitaji maalumu
- Upungufu wa miundombinu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum
- Upungufu wa walimu wenye taaluma ya elimu maalum

5.0 UTATUZI

- Kuhamasisha wazazi kuchangia Ujenzi wa Madarasa na Nyumba za walimu.
- Kutoa taarifa kwa ngazi husika kuhusu upungufu wa Walimu wenye taaluma ya elimu maalum pamoja na walimu wa kawaida.
- Kushirikisha wadau mbalimbali kusaidia kuboresha miundombinu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Naomba Kuwasilisha

PASCHAL BEREGE

AFISA ELIMU MSINGI

HALMASHAURI YA WILAYA MLELE